

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE

01

KISWAHILI

Muda: Saa 1:20

MAJIBU

Mwaka: 2023

Maelekezo

1. Karatasi hii ina jumla ya maswali **matano (5)**
2. Jibu maswali **yote**.
3. Andika majibu yote kwenye nafasi zilizoachwa wazi katika kila swali.
4. Andika majibu yote kwa kutumia kalamu ya wino wa **bluu** au **mweusi**

maktaba.tetea.org



SEHEMU A: IMLA (ALAMA 10)

1. Sikiliza kwa makini sentensi zifuatazo kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.
 - (i) **Nywele zako ni fupi.**
 - (ii) **Gharama ya umeme imezidi.**
 - (iii) **Mheshimiwa Rais amehutubia bunge.**
 - (iv) **Amesimama ng'ambo ya mto.**
 - (v) **Ndoo hii ni chafu.**

SEHEMU B: NYAKATI MBALIMBALI (ALAMA 10)

2. Sentensi zifuatazo zipo katika wakati gani? Andika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi. Sentensi (i) imetumika kama mfano.
 - i) Kaka anaimba nyimbo vizuri.
Wakati uliopo
 - ii) Daktari alimtibu mgonjwa wetu.
Wakati uliopita
 - iii) Baba yangu ataandika barua.
Wakati ujao
 - iv) Wanafunzi wanafanya mtihani wao.
Wakati uliopo
 - v) Kuku walitaga mayai mengi.
Wakati uliopita
 - vi) Baba na mama watalima shamba lote.
Wakati ujao

SEHEMU C: KUTEGUA VITENDAWILI (ALAMA 10)

3. Kamilisha vitendawili vifuatavyo kwa kuchagua maneno yaliyopo kwenye mabano na kuyaandika katika nafasi zilizoachwa wazi.

i) Askari wangu mpole lakini adui wanamhara _____ (paka, mbwa, mbuzi)

Mbwa

ii) Bibi hachoki kunibeba _____ (kiti, kochi, kitanda)

Kiti

iii) Nyumba yangu ina nguzo moja _____ (kalamu, uyoga, mlango)

Uyoga

iv) Mzungu katoka Ulaya na mkono kiunoni _____ (mkoba, ndoo, kikombe)

Mkoba

v) Tajiri wa rangi _____ (nyumba, mawingu, kinyonga)

Kinyonga

SEHEMU D: UTUNGAJI (ALAMA 10)

4. Sentensi zifuatazo zimechanganywa. Zipange katika mtiririko unaoleta maana kwa kuandika herufi A, B, C, D, E na F katika nafasi ulizopewa. Sentensi ya (i) imetumika kama mfano.

i) Hatimaye Kaposo alipelekwa hospitali. **F**

ii) Nyuki walikasirika, wakamfukuza na kumuuma Kaposo. **E**

iii) Siku moja Kaposo alitoroka shule na kwenda msituni. **A**

iv) Alirusha jiwe likapiga kwenye mzinga wa nyuki. **D**

v) Alikuwa akitumia manati yake kuwinda ndege. **C**

vi) Huko msituni Kaposo alikwenda kuwinda ndege. **B**

SEHEMU E: UFAHAMU (ALAMA 10)

5. Soma kwa makini shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu lililo sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

Uhai wa binadamu, wategemea mimea,
Mazingira ni muhimu, hakika twategemea,
Miti yetu ni adhimu, mvua twajipatia,
Pokea zangu salamu, tuhifadhi mazingira.
Kukulinda ni muhimu, miti yetu asilia,
Juhudi kila awamu, kuitunza asilia,
Miti ni zao muhimu, samani twajipatia,
Pokea zangu salamu, tuhifadhi mazingira.
Tumeishika hatamu, azima kuifikia,
Shughuli za binadamu, hakika zinachangia,
Kuuharibu utamu, wa miti na hewa pia,
Pokea zangu salamu, tuhifadhi mazingira.

a) Mwandishi wa shairi anasisitiza tulitunze zao gani?

Anasisitiza tulitunze **miti**.

b) Taja faida mbili tunazozipata kutokana na kutunza miti.

i) Tunapata **mvua**.

ii) Tunapata **samani**.

c) Nini kinasababisha uharibifu wa mazingira?

Uharibifu wa mazingira unasababishwa na **shughuli za binadamu**.

d) Nini maana ya neno “samani”?

Samani ni **vifaa vya nyumbani kama meza, viti na makabati**.

e) Katika ubeti wa pili mwandishi anatoa ujumbe gani?

Ujumbe ni **kulinda na kutunza miti ya asili kwa juhudi za pamoja.**